

https://doi.org/10.58256/qkmf2486

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 8, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 19th January 2024
Accepted: 16th March 2024
Published: 13th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

ISSN: 2520-4009 (Print)
ISSN: 2523-0948 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code

# Relationship between language and class: An analysis of the novels *Kuli* and *Pendo la Karaha*

**Virginia Wambui Mwathi, Vifu Makoti and John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: virginiamwathi6@gmail.com
https://orcid.org/0000-0002-5054-1740

**Abstract**
This paper investigates the relationship between language and class in reference to the novels *Kuli* (Shafi, 1979) and *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Language plays major roles in the society, that of being a tool of communication, an identifier of a person's geographical origin, rank amongst others. Further, language depicts the nature of relationship between speakers, gender and social class of a speaker. Our society has an entrenched economic system that has caused division and grouping of individuals into social classes according to their ability to own and control means of production. These social classes never fail to interact whenever their bids to seek livelihoods. When they interact, it is imperative that they use language. In view of this, in this article, we will interogate the type of communication and how it serves to aid in placing an individual in a particular social class: upper or lower social class.

Key words: Language,social class, hierarchy, status

**How to Cite:**
Mwathi, V. W., Makoti, V., & Mutua, J. (2024). Uhusiano wa Lugha na Tabaka: Uchanganuzi wa Riwaya za Kuli na Pendo la Karaha. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences, 8*(1). https://doi.org/10.58256/qkmf2486

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences

NJHS

https://doi.org/10.58256/qkmf2486

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 8, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 19th January 2024
Accepted: 16th March 2024
Published: 13th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

ISSN: 2520-4009 (Print)
ISSN: 2523-0948 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Mwathi, V. W., Makoti, V., & Mutua, J. (2024). Uhusiano wa Lugha na Tabaka: Uchanganuzi wa Riwaya za Kuli na Pendo la Karaha. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences*, *8*(1). https://doi.org/10.58256/qkmf2486

# Uhusiano wa Lugha na Tabaka: Uchanganuzi wa Riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha*

**Virginia Wambui Mwathi, Vifu Makoti and John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: virginiamwathi6@gmail.com
https://orcid.org/0000-0002-5054-1740

**Ikisiri**

Makala hii inachunguza uhusiano uliopo kati ya lugha na tabaka kwa mujibu wa riwaya za *Kuli* (Shafi, 1979) na *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Lugha ina jukumu muhimu katika jamii ambalo ni kufanikisha mawasiliano; hutumika kuwasilisha habari na hisia za watu. Kando na kuwa chombo cha mawasiliano, lugha hutambulisha: eneo atokalo mtu, cheo chake, na kadhalika. Vilevile, lugha huonyesha mahusiano ni ya aina gani baina ya wazungumzaji, jinsia na tabaka la mzungumzaji. Jamii tuliyomo ina mfumo wa kiuchumi ambao umegawa watu katika matabaka tofauti kulingana na uwezo wao wa kumiliki na kudhibiti njia za uzalishaji mali. Matabaka haya hayakosi kutangamana katika mchakato wa kutafuta riziki. Yanapotangamana, sharti lugha itumike. Kwa hivyo, katika makala hii, tutadadisi aina ya mazungumzo ya mtu ambayo humweka ama katika tabaka la juu au la chini.

**Istilahi muhimu:** Lugha, tabaka, itifaki,hadhi

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

**Utangulizi**

Lugha hutumika na jamii kuwasiliana. Katika jamii, kuna matumizi ya lugha kulingana na maeneo ya kijiografia, kitaaluma, kiuana, kiumri, kitabaka na kadhalika. Vilevile, kuna athari za uteuzi wa maneno kwa sababu ya mambo kadhaa kama vile: muktadha, jinsia, umri, uhusiano wa kiaila, itifaki kazini, rangi na kiwango cha urafiki. Aidha, uhusiano wa wanaozungumza huathiri uteuzi wa maneno. Kwa mfano, uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi, hadhi ya mtu katika jamii miongoni mwa mengineyo (Wardhaugh, 1997). Wardhaugh anaendelea kudai kuwa, uteuzi wa kiisimu wa msemaji, huakisi mahusiano ya kijamii ambayo msemaji anajua yanaishi kati yake na msikilizaji. Kwa mfano, mtoto anapozungumza na mzazi, atatumia lugha ya heshima kwa vile anajua kuwa mzazi ana hadhi ya juu kijamii kuliko mwanawe. Hii ni tofauti na mtoto anapozungumza na rafiki yake ambapo hutumia lugha ya kawaida. Vilevile, msimamizi wa kampuni atatumia lugha ya kuamrisha anapozungumzia mfanyakazi wake huku mfanyakazi akijibu kwa kunyenyekea. Mifano hii, kando na kudhihirisha mahusiano ya kijamii yaliyopo kati ya wazungumzaji, inaonyesha kuwa wazungumzaji wanaweza kudhihirisha utabaka kwa namna wanavyozungumza.

Makala hii, inanuia kuchanganua namna matumizi ya lugha hudhihirisha tabaka la mzungumzaji. Odetola na Ademola (1987) wanaeleza viashiria vya utabaka. Hivi ni kama vile: mapato na utajiri, kiwango cha elimu, kazi, makaazi, rangi na kabila. Kwa mujibu wa wataalam kama vile Wardhaugh (1997), Mc Gregor (2009), Coulmas (2013), na wengineo, tunakubali kuwa matumizi ya lugha ya mtu ni kiashiria cha tabaka lake.

**Muhtasari wa Riwaya ya *Kuli***

Riwaya ya *Kuli* (Shafi, 1979) ni hadithi inayosimulia hali ya Maisha ya Zanzibar chini ya utawala wa Waingereza. Shafi anasimulia mapambano kati ya makuli na wakuu wao na watawala. Katika jamii ya *Kuli,* rangi ya mtu inamweka katika tabaka fulani. Waafrika wanajipata katika tabaka la chini ambalo ni la wafanyakazi huku Waingereza wakiwa katika tabaka la juu ambalo ni tabaka la waajiri na watawala. Kazi ya ukuli ni ngumu sana iliyojaa hatari na ajali nyingi. Makuli wanatetea nyongeza ya mishahara kwa vile gharama ya maisha imepanda, malipo kwa kufanya kazi kwa saa za ziada, nguo za kazi na dhamana kwa kila mfanyakazi. Kwa jumla, ni riwaya inayosimulia harakati za Waafrika za kujikomboa kiuchumi na kisiasa chini ya utawala wa Waingereza.

**Muhtasari wa Riwaya ya *Pendo la Karaha***

Riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014) ni hadithi ya kusisimua inayoonyesha harakati za kujikomboa kiuchumi. Habwe anaonyesha matukio ya umaskini na utajiri. Kupitia kwa wahusika kama Kudra na Rukia, Habwe anasimulia namna umaskini na ukosefu wa ajira nchini Kenya unavyowasukuma kutafuta ajira ng'ambo. Wakiwa ng'ambo, wanaweza kukomboa familia zao kutoka kwa umaskini ingawa wanapitia changamoto tele. Vilevile, tunaelezwa namna serikali inavyofumbia macho matendo ya unyanyasaji unaotekelezwa na tabaka la juu. Kwa ufupi, ni riwaya inayomulika matatizo yanayokumba vijana wa karne ya 21 na juhudi zao za kujikomboa.

**Lugha na Tabaka**

Lugha ni kiashiria kikubwa cha tabaka kwa vile humulika nasaba za kitamaduni na kiuchumi-jamii za watu. Wanaisimu kama vile Labov (1966) anadai kuwa sifa za kiisimu kama vile matamshi, misamiati na sarufi, mara nyingi hutofautiana baina ya matabaka. Kwa mfano, mifumo fulani ya usemi ama lafudhi inaweza kuhusishwa na tabaka la wafanyakazi huku mifumo mingine ikihusishwa na watu wenye hadhi za juu katika jamii.

Bernstein (1971) anashadidia mjadala huu kwa kudokeza kuwa kuna uhusiano baina ya lugha na uhamaji wa utabaka. Anadai kuwa lugha inayotumika na watu inaweza kuwa na athari katika uhamaji wa utabaka na hata nafasi za kujiendeleza. Nadharia ya Bernstein ya ubadilishaji wa msimbo inadhihirisha

namna watu kutoka matabaka tofauti wanavyoweza kubadilisha msimbo kulingana na muktadha waliomo. Kwa mfano, anayetoka tabaka la wafanyakazi, anaweza kubadilisha mfumo wa usemi wake anapotangamana na watu katika miktadha rasmi ama ya kitaaluma ili mfumo wake wa usemi uoane na kaida za tabaka la kati, na hivyo kuimarisha uhamaji wa utabaka.

Bourdieu (1991) anadai kuwa umilisi wa lugha na ufahamu wa lafudhi au rejista inayotawala, unaweza kuleta manufaa katika jamii. Watu wenye ufahamu na umilisi wa lugha inayotumika na tabaka tawala wanaweza kupata nafasi bora za elimu na kitaaluma kuliko wasio na ufahamu na umilisi huu. Hii huendeleza zaidi ukosefu wa usawa katika jamii. Hii ni kuwa wale watokao nasaba za chini kiuchumi, wanaweza kukumbana na vikwazo vya kiisimu wanapojaribu kupenya katika mifumo ya uwezo na yenye mapendeleo. Lippi- Green ( 2012) anakubaliana na madai ya Bourdieu kwa kudokeza kuwa, tafiti zinaonyesha lugha inaweza kuwa na athari katika kupatikana kwa ajira. Katika mahojiano ya kikazi, iligunduliwa kuwa, watafutaji wa kazi waliotumia lugha sanifu walionekana kama wenye akili zaidi kuliko waliotumia iliyokuwa si sanifu licha ya sifa zao zingine kuwa sawa.

**Uhusiano wa lugha, Elimu na Tabaka**

Cameron (1995) anadai kuwa, matumizi ya lugha sanifu au 'sahihi' yanahusishwa na watu walioelimika. Hiki ni kichocheo cha utabaka. Anaendelea kudai kuwa, watu wasiozungumza Kiingereza sanifu huonekana kuwa wenye elimu ya kiwango cha chini hata kama wana usanifu katika lugha zingine. Kwa maoni yetu, usanifu katika lugha ya Kiingereza hautoshi kuwa kiashiria cha kiwango cha elimu ya mtu na hata tabaka lake. Kuna watu ambao hujivunia lugha zao za kitaifa kama vile Kifaransa, Kijerumani, Kihispania, Kiganda na kadhalika, wakazisoma katika viwango tofauti vya elimu na kuzitumia katika taaluma zao. Si ajabu kupata daktari asiyezungumza Kiingereza sanifu lakini anafanya kazi yake barabara. Hii haimaanishi kuwa daktari huyu hana elimu ya hali ya juu. Aidha, haimaanishi yu katika tabaka la chini.

Namna nyingine ambayo lugha huonekana kama kiashiria cha kiwango cha elimu na tabaka, ni katika matumizi ya msamiati wa pekee hasa miongoni mwa wataalam ama makundi ya kijamii. Kwa mfano, mawakili, madaktari na wanasayansi wanaweza wakatumia misamiati ya nyanja zao isioeleweka na watu wasio wataalam (Bourdieu, 1986). Hawa ni watu ambao taaluma zao zina fahari ya kikazi ya kiwango cha juu katika jamii na hivyo katika matumizi ya lugha, kutumia misamiati ya kipekee ya taaluma zao kunawaweka katika tabaka la kati au juu.

Kutokana na madai ya wataalam hawa, inaonekana kuwa, uzungumzaji wa lugha sanifu unahusishwa na elimu ya kiwango cha juu. Ifahamike kuwa, ili kupata elimu ya kiwango cha juu, mfano nchini Kenya, sharti uwe na uwezo mkubwa hasa wa kiuchumi ili kuweza kuimudu. Kwa hivyo, ni kweli kusema kuwa kuna uhusiano kati ya lugha, elimu na tabaka.

Yule (2017) anashadidia kwa kudai kuwa, watu wanaoishi katika jamii moja lakini wana tofauti ya kielimu na kiuchumi, huzungumza kwa njia tofauti. Tofauti hizi zinaweza zikatumika kama kiashiria cha ushirika wa mtu katika kundi fulani la kijamii ama jamii fulani ya wazungumzaji. Kwa hivyo, tunaamini kuwa, uhusiano wa watu katika jamii unaathiri matumizi yao ya lugha na hivyo basi kuakisi tabaka la mtu. Coulmas (2013: 20) ana madai yafuatayo kuhusu matumizi ya lugha:

i. Huonyesha nafasi ya mzungumzaji katika jamii.
ii. Wazungumzaji hubadili vitabia vyao vya uzungumzaji kulingana na wanavyozungumziwa.
iii. Wazungumzaji hubadili vitabia vya uzungumzaji kulingana na hali ama tukio fulani katika jamii.

Madai ya Coulmas yatatusaidia katika kudhihirisha tabaka la mzungumzaji na sababu ya mzungumzaji kuzungumza kwa namna fulani.

**Uhusiano wa lugha na Tabaka katika Riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha***

Katika utafiti huu, tumegundua kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha na tabaka, hasa katika mazingira ya

kazini ambapo kuna itifaki kazini na hata katika muktadha wa utawala. Uhusiano kati ya wazungumzaji katika mazingira haya, unaakisi pengo lililopo kati ya tabaka la mwajiri na mwajiriwa. Cheo au mamlaka ya mtu yanamlazimu kutumia lugha kwa njia fulani. Kwa hivyo, uhusiano kati ya wazungumzaji ni kichocheo kikubwa katika matumizi ya lugha. Mwajiri au mtawala anapozungumza, lugha yake inaweza kuwa ya kutoa amri, vitisho, dharau na kiburi, ukali na hata matusi. Hii ni tofauti na ile ya mwajiriwa au mtawaliwa ambapo mara nyingi huwa yenye unyenyekevu, woga na inayodhihirisha heshima kwa mwajiri wake. Hii inaonyesha ukweli wa madai ya McGregor (2009) kuwa, miundo kadhaa ya kiisimu pamoja na vitabia ambavyo wazungumzaji hutumia, huwakilisha utambulisho wao. Miundo hii ya kiisimu na vitabia hivi huonyesha mzungumzaji ni nani. Kwa kuonyesha msemaji ni nani, tunaweza kafahamu nafasi yake katika muktadha huo wa mazungumzo.

Uhusiano wa lugha na tabaka unajitokeza katika riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha*. Kuna muktadha wa kazini na wa utawala ambako wahusika ni mwajiri na mwajiriwa na mtawala na mtawaliwa. Vilevile, kuna matumizi tofauti ya lugha kutokana na itifaki hii. Matumizi haya ya lugha, yanamweka mzungumzaji katika tabaka fulani, ama la juu au la chini.

Katika riwaya ya *Kuli,* kuna matumizi ya lugha yanayoakisi tabaka la mzungumzaji.

**Muktadha wa Kazini**

Kule gatini, tunaona namna Mshihiri ambaye ni mwajiri na msimamizi wa wafanyakazi anavyotoa maelekezo ya kazi kwa wafanyakazi wake.

> Mfano 1
> "Washa maskhara yako weye, lazma kikapu nayaza tele," Mshihiri alimwambia mmoja wa wale wachukuzi.
>
> (uk.13)

Katika kampuni ya Smith Mackenzie, chini ya George ambaye ni meneja anayesimamia makuli, tunapata dondoo lifuatalo:

> Mfano 2
> "Hapana wacha sanduku naanguka wewe! Kamata na mkono mpaka sanduku nafika chini!" George alitoa amri kwa sauti kubwa... " Mimi nasema kamata sanduku mzuri wewe nacheza hapa!"
>
> (uk.61)

Mfano 1 na 2, ni lugha ya kuamrisha na yenye ukali. Lugha ya kuamrisha inadhihirisha kuwa, anayeitumia ni msimamizi au mwajiri. Hapa, tunaona kuwa Mshihiri na George wamewasimamia wachukuzi katika kazi ile ya ukuli. Tunakubaliana na madai ya Coulmas (*kama hapo juu*) kuhusu matumizi ya lugha. Lugha ya Mshihiri na George inadhihirisha kuwa wao wana hadhi ya juu kikazi kuliko wafanyakazi wao. Hii ni kwa vile ni lugha ya kuamrisha na yenye ukali. Pamoja na hayo, tabia ya Mshihiri na George ya kuamrisha ni kutokana na hali ya kutaka kazi kufanyika na kukamilika kwa njia wapendayo.

> Mfano 3
> "Wee kalb wee! Weye nashkua kibati mara mbili kwa kikabu moya," mara yule Mshihiri aliyakatiza mazungumzo yake na Rashidi na kumgeukia mfanyakazi mmoja...
>
> (uk.15)

Katika dondoo hili, maneno ya Mshihiri kwa mfanyakazi ni yenye matusi. Kutusi mtu kunamaanisha kuwa unamdunisha. Fauka ya hayo, katika mazingira kama haya ya kazini, yanadhihirisha kuwa Mshihiri yu katika hadhi ya juu kuliko mfanyakazi wake kwa vile anatumia cheo chake kumtusi mfanyakazi yule.

**Muktadha wa Utawala**

Katika muktadha wa utawala, lugha kati ya mtawala na mtawaliwa inadhihirisha utabaka. Katika ofisi ya Kamishna ambaye ni mkuu wa polisi, tunaona mazungumzo kati ya Kamishna na Ubwa na Chum. Ubwa na Chum wanamwendea Kamishna kumsihi kuwafungulia makuli waliokamatwa wakati wa mgomo wa makuli.

> Mfano 4
> "Mimi nauliza nyinyi nataka nini hapa?' Kamishna aliuliza tena, sasa kwa hamaki macho ameyatumbua huku uso umemuiva...
> "Sisi hatukujia ugomvi Bwana Mkubwa. Sisi tumekuja kukuomba wale wenzetu waliotiwa ndani watolewe," Ubwa alisema kwa sauti ya huruma na unyenyekevu.
> "Ile wenzenu haitoki na kama ile watu mingine nafanya fujo na wao takwenda *jail* vilevile!"
> "*Listen you fools!* Wale wenzenu haiwezi kutoka mpaka kwa amri ya Bwana *Resident* na kama nyinyi tafanya fujo zaidi sisi tatia ndani ninyi yote,"
> (uk.92)

Matumizi ya lugha ya Kamishna katika dondoo hili, ni yenye ukali na vitisho. Kwa kusema, "...na kama nyinyi tafanya fujo zaidi sisi tatia ndani ninyi yote," inadhihirisha vitisho. Aidha, kuwaita '*fools',* kunaonyesha kuwa Kamishna ni mwenye matusi. Ubwa, kama mwajiriwa, anatumia lugha yenye huruma na unyenyekevu. Hii inadhihirisha heshima yake kwa wakubwa wake.

Katika ofisi kuu ya Kampuni ya Smith Mackenzie, tunaendelea kuona mazungumzo ya Mzungu ambaye ni mmoja wa wakuu wa kampuni hii, akizungumzia Faraji ambaye ni mwakilishi wa makuli kuhusu mgomo wa makuli.

> Mfano 5
> "Sikiliza!" Alianza yule mzungu ambaye alikuwa anakabiliana uso kwa uso na Faraji, "Unajua kama nyinyi hapana kutaka kufanya kazi iko watu mingi hapa mjini Zanzibar naranda ovyo kama mbuzi na sisi naweza chukua wao kazini?"
> (uk.96)

Dondoo hili vilevile linadhihirisha vitisho. Mzungu anaposema, "...iko watu mingi hapa mjini Zanzibar naranda ovyo kama mbuzi na sisi naweza chukua wao kazini," inaonyesha bezo na vitisho, namna anavyowafananisha maskini na mbuzi. Aidha, ni kuwatisha kuwa watapoteza ajira yao wasiporudi kazini. Kwa mujibu wa madai ya Coulmas (2013), tunaweza kusema kuwa lugha ya Kamishna katika mfano 4 na Mzungu katika mfano 5, inadhihirisha kuwa wao wana hadhi ya juu kuliko waajiriwa kwani ni yenye ukali, matusi na vitisho. Unyenyekevu wa Ubwa kwa Kamishna unadhihirisha kuwa yuko chini kihadhi katika maongezi yao. Kwa hivyo, lugha imedhihirisha hadhi ya mzungumzaji. Pamoja na hayo, hali iliyopo ya tofauti na kutoelewana kati ya waajiri na watawala kwa upande mmoja, na makuli kwa upande mwingine, inamlazimu Ubwa kuwa mnyenyekevu ili ombi lake la kutaka wenzake wafunguliwe kutoka jela lijibiwe na Kamishna. Fauka ya hayo, tunaamni kuwa hali ya mgomo iliyopo inamfanya Mzungu atumie lugha ya vitisho ili kufanya wafanyakazi wawe na woga na waridhie kurudi kazini.

> Mfano 6
>
> Kiongozi wa mashitaka aliendelea na maswali yake. "Wewe Rashidi bin Majaliwa unakataa kama hukusababisha ghasia huko gatini mpumbavu wewe?"... "*You!* Mpumbavu! Sasa hivi umesema unajua kwamba ukimshambulia ofisa wa polisi, ilhali umevaa yunifomu ni kosa kubwa..."
>
> (kur. 187 & 189)

Dondoo hili linaonyesha mazungumzo kati ya Rashidi na kiongozi wa mashitaka wakiwa kotini. Hii ni baada ya Rashidi kukamatwa kwa kuhusika katika mgomo na kumshambulia ofisa wa polisi. Rashidi kuitwa mpumbavu, ni matusi. Matusi hudhihirisha udunishaji. Fauka ya hayo, ni kumwonyesha Rashidi kuwa yu chini kihadhi akilinganishwa na kiongozi wa mashtaka. Tunahusisha matusi na watu wa tabaka la juu wanapowazungumzia wale wa tabaka la chini. Tunaamini kuwa wao hutumia matusi kwa vile wao ndio hudhibiti utawala na uchumi, kwa hivyo hawana wa kuwatisha. Aidha, tabaka la chini linaweza kukosa kutumia matusi linapozungumzia lile la juu kwa sababu linaweza likaharibu uhusiano katika yao na hivyo kupoteza namna ya kupata riziki kwa vile hutegemea lile la juu kupata riziki baada ya kufanya kazi. Aidha, katika muktadha wa utawala, wanaweza kujipata wakifungwa kwa sababu ya matusi na kwa sababu ya kutokuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi, wanaweza kukosa uwezo wa kujiondoa katika matatizo kama haya.

Katika dondoo hizi, inadhihirika kuwa Kiswahili cha Mshihiri, Kamishna, Mzungu na kiongozi wa mashtaka si sanifu. Ingawa lugha sanifu huhusishwa na tabaka la juu, ambalo ni tabaka la hawa watatu, lugha yao si sanifu kwa vile wao ni wageni katika sehemu hii ya Zanzibar, na Kiswahili si lugha yao ya kwanza. Wamejifunza tu kwa minajili ya kutangamana na wenyeji lakini hawajapata umilisi. Tunakubaliana na madai ya mwanaisimu Noam Chomsky, kuwa hakuna mtu duniani anayejifunza lugha ya pili (L2) kufikia kiwango cha kuifahamu kama lugha ya kwanza (L1). Kwa hivyo, mtu huwa na umilisi wa lugha ya kwanza kuliko ya pili (Vivian na Newson, 2007).

Katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* uhusiano wa lugha na tabaka unadhihirika kama ifuatavyo:

**Muktadha wa Kazini**

Nyumbani mwa Nayrat, tunapata mazungumzo kati ya Nayrat na Kudra. Kudra ni mfanyakazi wa Nayrat na anaonywa dhidi ya kuzungumza na majirani baada ya Nayrat kumpata akiamkua jirani.

> Mfano 7
>
> "Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe," Nayrat alisema kwa sauti ya ukali...
> "Nilikuwa namwamkua tu yule jirani," Kudra alisema.
> "Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?" Nayrat aliuliza.
> "Pole, sitarudia tena," Kudra alitamka radhi.
>
> (uk.94)

Matamshi ya Nayrat katika dondoo hili ni yenye kuamrisha huku ya Kudra yakidhihirisha unyenyekevu. Kuamrisha kwa Nayrat kunadhihirisha kuwa yuko juu kihadhi kuliko Kudra. Vilevile, hali ya Nayrat ya kutaka Kudra amtii na asirudie kosa inafanya atumie lugha ya kuamrisha. Pamoja na hayo, unyenyekevu wa Kudra kwa Nayrat kunaonyesha kuwa yuko chini kihadhi na pia kunaonyesha hali ya kutotaka kumkosea mwajiri wake na mwishowe aipoteze kazi yake.

Kudra kuzungumziwa kwa ukali na Nayrat, kunamlazimu yeye kunyenyekea ili hali iliyopo kati yake na Nayrat isiharibike zaidi ya ilivyo. Kwa hivyo, kunyenyekea kwake kunatokana na anavyozungumziwa

kwa ukali na Nayrat.

Aidha, tunaona mazungumzo kati ya Kudra na Saumu ambaye ni msimamizi wa wafanyakazi katika *massage parlour* ya Fauziya. Mazungumzo haya yanatokea baada ya Saumu kuona kuwa Kudra analegea katika utendakazi wake.

> Mfano 8
> "Dadangu, mbona hutaki kufuata maagizo ya kazi?" Saumu alimwuliza Kudra.
> "Mimi kazi hiyo siipendi, sitaki kuifanya," Kudra alisema.
> "Lazima utaifanya. Ikiwa hutaki kuifanya, nitakufanya uifanye!" Saumu alisema kwa hasira.
> Saumu alimtolea maneno yenye sumu kali, "Unaleta mchezo hapa? Wewe unadhani ni bora kuliko sisi? Pana wasichana warembo hapa. Ikiwa unadhani ulikuja raha, sahau. Ulikuja kufanya kazi. Ukichagua kazi ni shida yako. Mimi sitavumilia kiburi chako, unasikia?"
> "Ndiyo, ninasikia," Kudra aliyesinasina alisema.
> (kur.165-166)

Maneno ya Saumu katika dondoo hili ni yenye vitisho. Vitisho hivi vinamkumbusha Kudra kuwa yeye ni mwajiriwa na hana budi ila kufanya kazi kama inavyotakikana. Vitisho hivi vinadhihirisha pia kuwa Saumu yuko juu kihadhi kuliko Kudra.

Baada ya Riziki kusikia kuwa mwanawe (Kudra) anatesekea Dubai, anaenda kumwona Rehema katika ofisi yake. Rehema ni wakala aliyesafirisha Kudra. Tunapata mazungumzo kati yao kuhusu suala hili.

> Mfano 9
>
> "Mwanangu ulimpeleka Dubai sasa nasikia anafanyiwa mateso huko," Riziki aliteta.
> " Mwanao alienda kwa hiari yake, dadangu. Pia akiona si kuzuri, ana miguu na macho. Anaweza kurudi. Kama umechomwa na hasira, nenda polisi. Nenda unishtaki," Rehema alimweleza Riziki…
> (kur.169-170)

Maneno ya Rehema katika dondoo hili yamejaa kiburi. Kwa kusema, "...nenda polisi...nenda unishtaki," anaonyesha namna alivyo jasiri na kutokana na haya, ni kweli kusema kuwa ujasiri wake unatokana na uwezo wake mkubwa wa kiuchumi unaompa 'haki' ya kutamka maneno kiholela kwa vile mali yake ni 'ngao' yake. Kiburi cha Rehema kinatokana na hali ya kutaka kuonyesha Riziki kuwa hatishwi na chochote. Aidha, kinaonyesha kuwa yuko juu kihadhi kuliko kuliko Riziki.

**Mazungumzo kati ya Watu wa Tabaka Moja**

Kando na kuchunguza mazungumzo kati ya watu wa matabaka tofauti, tulichunguza pia mazungumzo kati ya watu wa tabaka moja. Tulitaka kudhihirisha ikiwa yana sifa sawa na yale ya watu wa matabaka tofauti ama yana sifa ya kipekee. Katika riwaya zote mbili, tulipata mazungumzo katika ya watu wa tabaka la wafanyakazi tu. Mawasiliano kati ya watu wa tabaka moja yana maana ya kupitisha habari, maoni na jumbe kati ya watu au makundi yaliyo katika itifaki sawa ama kati ya idara tofauti kwenye shirika moja. Mawasiliano kama haya hufanyika kati ya makundi ambayo hayapo katika uhusiano wa msimamizi au mwajiri- mfanyakazi. Mawasiliano kama haya husaidia katika uratibu kazini, ushirikiano, usuluhishaji wa matatizo na hata mchakato wa kufanya uamuzi (Robbins na Judge, 2019).

Luthans (2019) anadai kuwa mawasiliano kati ya watu walio katika itifaki sawa hukuza ushirikiano baina ya wafanyakazi. Hii huongeza kiwango chao cha kutosheka kikazi na uaminifu kazini. Sifa hii huzaa utamaduni chanya wa kikazi.

Hata hivyo, mawasiliano ya aina hii yanaweza kuwa na changamoto. Changamoto hizi ni kama vile: kutoeleweka au kuvurugwa kwa habari au jumbe. Hii ni kwa vile aina hii ya mawasiliano haifuati itifaki ya kutoka juu kwenda chini (msimamizi-mfanyakazi). Zaidi ya hayo, migogoro inaweza kuzuka ikiwa kuna tofauti za malengo, mitazamo na vipaumbele kati ya wafanyakazi.

Katika riwaya ya *Kuli*, tunapata dondoo zifuatazo:

> Mfano 10
> " Unajua weye," Farjalla alianza, " Mie leo nimefika hapa mapema zaidi kusudi nipate kuongea na wewe faragha. Yale maneno uliyoyasema jana juu ya kazi tunayofanya na malipo tunayopata ni maneno madhubuti sana. Sisi sote tunakubaliana nayo na kila siku sisi hutaka kumwambia Mzee Tindo lakini tunaogopa asije akamtilia mtu kitumbua chake mchanga."
> " Kwani yeye Mzee Tindo hataki pesa zaidi? Rashidi aliuliza.
> "Ah! Yeye anapata pesa zaidi kuliko sisi hata mbali ya zile anazochukua zinazozidi hapa, ujira wake..."
>
> (uk.45)

Haya ni mazungumzo kati ya Rashidi na Farjalla wakiwa katika mazingira ya kazini. Wanazungumzia suala la malipo yao ambayo ni madogo. Wote wawili ni wafanyakazi wa kiwango sawa. Kutokana na mazungumzo yao, inadhihirika kuwa ni mazungumzo yenye sifa ya uwazi. Hakuna anayeogopa mwingine kati ya wawili hawa ingawa Farjalla anaogopa msimamizi wa ambaye ni Mzee Tindo. Hii inatokana na yeye kusema kuwa amefika mapema ili azungumze na Rashidi faragha na kukiri kuwa yeye na wafanyakazi wengine wanamwogopa Mzee huyu. Aidha, mazungumzo yao yanakatizwa na mjo wa Mzee Tindo (uk.45). Kutokana na hayo, Rashidi na Farjalla wanatokea kuwa wenye uwazi na ni wasiri. Hakuna anayeonekana kumdhibiti mwingine.

> Mfano 11
> "Hii kazi hii! Hii kazi ya kitumwa hii!" alisema kuli mmoja...
> "Hawa wanatutumia kama punda na kila tunapowaambia habari ya nyongeza ya malipo wanatutia huku wakitutoa huku! Aliongeza kuli mwingine.
> "Kwani nyie hamwogopi kudai pesa zaidi huku?" Rashidi aliuliza.
> Hakuna aliyemjali Rashidi.
>
> (uk.62)

Haya ni mazungumzo kati ya makuli wakiwa kazini. Haya ni mazingira mapya ya kazi kwa Rashidi baada ya kupoteza kazi yake chini ya Mzee Tindo kwa Morarji. Mazungumzo haya, sawa na yale ya kati ya Faraji na Rashidi, ni ya wafanyakazi wa kiwango kimoja. Makuli hawa wanaonekana kuwa na uwazi wanapoongea. Kwa kusema kuwa "Hii ni kazi ya kitumwa...wanatutumia kama punda" inadhihirisha makuli hawa wakiwa peke yao, hawana uoga wowote kuzungumzia yanayowakera kazini. Kuna uwazi katika mazungumzo yao. Sifa hii inawachora kama wasiri pia. Aidha, hakuna elementi za uamrishaji na unyeyekevu kati yao kwa vile ni watu wa kiwango kimoja.

Katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* mazungumzo kati ya watu wa tabaka sawa yanadhihirika.

Mfano 12

"Dadangu, nataka kutoka kwenye utumwa huu. Ninatajirisha watu. Wanaendesha *Mavolvo, Mercedes Benz, Malandrover, Discovery* na mimi mwenyewe ni mtumwa. Silali. Kisa na maana ni kuzungusha dawa angalau kumlipa mkubwa wangu. Dadangu usiwahi kuingia katika gari hili. Siku zote natazamia kushuka sijui nitashuka vipi. Huu ni utumwa..." Lindo alimweleza Kudra.

(uk.31-32)

Katika dondoo hili, maneno ya Lindo kwa Kudra yanaonyesha machungu yake kutokana na kazi anayoifanya. Kwa uwazi bila uoga, anamwambia Kudra namna alivyo mtumwa na anavyotamani kuwacha kazi hiyo. Maneno yake yanatokea kuwa ushauri kwa Kudra. Wawili hawa ni wa tabaka sawa ingawa Kudra hafanyi kazi ya kuuza dawa za kulevya. Maneno ya Lindo hayana elementi za uamrishaji ama unyenyekevu kwa vile yeye na Kudra ni wa kiwango sawa cha kiuchumi.

Mfano 13

"Dadangu utaamini kuwa huu mwezi ni wangu wa sita na sijapata mshahara?" Almasi alisema...

"Hata mimi ni hivyo. Ila mimi ninapewa elfu mbili za Kenya. Hizo nazo utafanyia nini?" Kudra aliuliza.

"Afadhali wewe. Mimi ninaomba nipewe hata shilingi moja tu," Almasi alisema...

"Lakini mimi nikipata mali yao, nitachota kisha nikimbie," Almasi alisema bila kuonyesha utani.

(kur.112-113)

Haya ni mazungumzo kati ya Almasi na Kudra. Wao ni wafanyakazi wa kazi za nyumbani, chini ya waajiri tofauti. Mazungumzo yao yanahusu kufahamishana kuhusu changamoto zao katika kazi zao. Kitendo cha Almasi kumwambia Kudra kuwa atachota mali ya waajiri wake kinaonyesha kuwa hamwogopi Kudra. Hivyo, mwandishi anawachora kama wasiri. Mazungumzo yao hayatokei kuwa na elementi za uamrishaji ama unyenyekeaji kwa vile wote ni wa kiwango sawa.

Kutokana na uchanganuzi wa mazungumzo kati ya watu wa tabaka moja, inadhihirika kuwa mazungumzo yao yana sifa ya uwazi na kutokuwepo kwa uoga wakati wa kuzungumza kuhusu changamoto zao na mipango yao. Mazungumzo yao yanaonekana kuwa kama udaku. Sifa hii inawachora kama wasiri. Tunapolinganisha mazungumzo yao na yale ya mwajiri na mwajiriwa ama mtawala na mtawaliwa, kuna tofauti. Mazungumzo kati ya watu wa matabaka tofauti yana sifa ya uamrishaji, kiburi,vitisho na matusi kwa upande wa mwajiri ama mtawala huku yale ya mtawaliwa ama mwajiriwa yakiwa yenye heshima na unyenyekevu. Tunaamini kuwa, ingawa riwaya teule hazikudhihirisha mazungumzo kati ya watu wa tabaka la juu, sifa zinazojitokeza katika mazungumzo ya watu wa tabaka la chini ndizo tu zitakazojitokeza kwa wale wa tabaka la juu. Watu wa tabaka la juu wanapoongea na wenzao wa tabaka la juu, hawataamrishana wala kutusiana ama kuonyeshana kiburi. Mazungumzo ya watu wa tabaka la juu yanaweza kuhusu uwekezaji huku ya wale wa tabaka la chini wakizungumzia matatizo yao ya kazini. Kwa hivyo, tunaweza kusema mazungumzo ya mtu ni kielekezi cha tabaka lake.

**Hitimisho**

Kutokana na matukio ya matumizi ya lugha katika riwaya hizi mbili, inadhihirika kuwa, watu wa tabaka la juu hutumia lugha ya kuamrisha, yenye vitisho, ukali, matusi, dharau na kiburi ili kudhihirisha hadhi yao katika jamii. Zaidi ya hayo, maneno haya ni yenye kumdunisha yule wa hadhi ya chini, kumfahamisha kuwa si wa hadhi sawa na yule wa juu na hivyo kumwonyesha kuwa sharti awe mnyenyekevu. Kwa hivyo,

matumizi ya lugha ya watu wa tabaka la juu huwasaidia kudumisha hadhi zao. Kwa upande mwingine, watu wa tabaka la chini hutumia lugha yenye huruma na unyenyekevu kwa vile wanafahamu kuwa, kutokana na hadhi yao katika jamii, ni sharti wanyenyekee ili kudumisha uhusiano wao na wakubwa wao. Inawabidi wawaheshimu wakubwa wao kwa vile wanawategemea kupata riziki. Kwa hivyo, huishi kwa hofu, wasiwakosee na mwishowe kupoteza kazi zao na hivyo kukosa riziki. Kutokana na haya, ni dhahiri kuwa lugha ni muhimu sana katika kuakisi tabaka la mtu katika jamii. Pamoja na hayo, tumeshughulikia matumizi ya lugha kati ya watu wa tabaka moja. Tumegundua kuwa ni lugha yenye sifa ya uwazi, kutokuwepo kwa uoga na inawachora wazungumzaji kama wasiri. Ni lugha isiyo na sifa za dharau, vitisho, matusi, kiburi, uamrishaji na unyenyekevu kama inavyodhihirika katika mazungumzo kati ya watu wa tabaka la juu na la chini. Haya yote ni kwa sababu hakuna anayemdhibiti mwingine na masilahi na changamoto zao zinafanana. Uchanganuzi wetu umepata, kando na lugha ya mtu kudhihirisha kiwango chake cha elimu na hivyo kuwa kielelezi cha tabaka la mtu, toni ya mzungumzaji na uteuzi wake wa maneno katika miktadha kama vile ya kazini na ya kiutawala ni kiashiria cha tabaka la mtu.

**Marejeleo**


Adam, S. (1979). *Kuli*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Bernstein, B. (1971). *Class, Codes and Control: Theoretical Studies Towards a Sociology of Language*. New York: Routledge.

Bourdieu, P. (1986). *The Forms of Capital. Handbook of Theory and Research for the Sociology of Education*. New York: Greenwood Press.

Bourdieu, P. (1991). *Language and Symbolic Power*. Cambridge, Massachusetts: Harvard University Press

Cameron, D. (1995). *Verbal Hygiene*. New York: Routledge.

Coulmas, F. (2013) *Sociolinguistics: The Study of Speakers' Choices*. United Kingdom: Cambridge University Press.

Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha*. Nairobi: Moran Publishers.

Labov, W. (1966). *The Social Stratification of English in New York City*. Washington, DC: Center for Applied Linguistics

Lippi-Green, R. (2012). *English with an Accent: Language, Ideology, and Discrimination in the United States*. New York: Routledge.

Luthans, F. (2019). *Organizational Behavior: An Evidence-Based Approach*. (13th Edition). New York: McGraw-Hill Education.

McGregor, W. (2009) *Linguistics: An Introduction*. Great Britain: Bloomsburry Publishing Plc.

Odetola, O., & Ademola, A. (1987). *Sociology: An Introductory African Text*. Hong Kong: Macmillan Publishers.

Robbins, P., & Judge, A. (2019). Essentials of Organizational Behavior (14th Edition). New York: Pearson

Vivian, C., & Newson, M. (2007). *Chomsky's Universal Grammar: An Introduction*. Hoboken: Blackwell Publishing.

Wardhaugh, R. (1997). *An Introduction to Sociolinguistics*. Great Britain: Blackwell Publishers.